# JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA
# GATUZI NDOGO YA KANDARA - KIDATO CHA TATU
## KISWAHILI (FASIHI)
Karatasi - 102/3
**Oktoba / Novemba - 2016**
## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**1. SABUNI YA ROHO.**

Maswali.

i) Taja nafsi nenewa. Thibitisha.
Nafsi nenewa ni pesa / fulusi - waja wanazitumiwa kusuluhisha matatizo mbalimbali kama vile kununulia vifaa kulipa madeni.

ii) Eleza toni ya nafsi neni (alama 1)
- Toni ya nafsi neni ni ya kulalamika. Analalamika kuwa pesa zimemkimbia.
- toni ya kusifia - ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

iii) Eleza arudhi zozote nne zilizozingatiwa katika utunzi wa shairi hili.
- Beti nne
- Mshororo minne katika kila mshororo.
- Vina vinabadilika katika kila ubeti isipokuwa kibwagizo
- Mshororo wa mwisho ni kibwagizo - sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

iv) Mshairi anawasilisha ujube gani katika mleo wa ubeti wa sita?
- Pesa zimeteka nyara roho za wapendanao na kuwafanya kuuana majumbani mwao.

v) Ukittoa mfano eleza mbinu zozote tatu za lugha alizotumia mshairi.
- Balagha - ewe tunu ya mtima, kwa nini wanikimbia?
- Tashbihi - sinilipe ja bomu.
- Jazanda - jehanamu ni tatizo.
- Tashisi - fulusi zinazoombwa kumwondoa mnenaji jehanamu, zina uchoyo.
- Takriri - ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

vi) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari.
Mshairi anamsihi mvunja mlima (pesa) kuwasaidia maskini na mayatima ambao hali zao duni. Awabebe waliokwa__ kuwainua walio chini. Ndiye sabuni ya roho na mvunja mlima (mtimiza yote).

vii) Jadili jinsi mshairi anatumia ruhusa ya mshairi.
- Inkisari - mfano; sinilipue - usinilipue. 'mefufua - umefufua.
- Kuboronga sarufi - mfano wema wako wameonja badala ya wameonjwa wema wako. Naondoka wangu moyo badala ya naondoka monyo wangu.

viii) Kwa kurejelea mpangilio wa vina eleza bahari ambamo shairi hili linaweza kuainishwa.
Bahari : Ukaraguni - kila ubeit una vina tofauti na vya ubeti mwingine. (alama 1)

ix) Fafanua maana ya:
i) Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.
- Ni wewe ambaye hufurahisha na kusuluhisha matatizo yote.

ii) Jehanamu.
- Tatizo

**2.a) Maneno ya Siki.**
- Anamwambia Meya.
- Walikuwa nyumbani kwa Meya.
- Siki alikuwa amekuja kumweleza Meya hali halisi ya mambo / kukosekana kwa madawa na matatizo mengine.
- Meya mwishowe aliamuru Gedi kumfurusha Siki.

**b)** Msemo - mambo kutonyooka - mambo kutokuwa sawa.

c)
- Huduma ya matibabu ni ya chini.
- Ukosefu wa ajira.

- Mishahara duni (walipata nusu)
- Mishahara kucheleweshwa
- Hali ngumu ya maisha baada ya gharama kupanda.
- Kukosa nyongeza kwa wafanyikazi wa chini.
- Makazi ya wanyonge yalikuwa mabanda.
- Maskini kutembea kwa miguu ilhali matajiri walibebwa kwa magari mazito yenye 'air conditioner'.
- Elimu duni kwa watoto maskini wanafukuziwa karo ilhali madiwani wanalipiwa na baraza.
- Wanaolipa kodi ni maskni (mama muuza ndizi)
- Kunyimwa haki ya kusikilizwa mfano wawakilishi wa wafanyi kazi.
- Ukosefu wa vifaa vya kufanya kazi - glovu.
- Wizi wa mali ya umma mfano: Vipande vya ardhi na Meya kwenda katika hoteli za kifahari akitumia Entertainment (ubadhirifu)
- Njama ya wizi wa fimbo ya Meya.
- Diwani III kutohusihswa kwenye mikutano.
- Waandamanaji kupigwa na polisi.
- Bibi ya Meya kwenda kujifungulia ngambo.
- Mhubiri kupewa sadaka na kufadhiliwa na baraza.
- Madiwani kununuliwa nguo na baraza.

*zozote 8 × 1 = 8*

**d)**

- **Siki** alienda kwa Meya kujaribu kumshawishi abadilishe uongozi wake.
- **Diwani** 3 alimuarifu Meya kuhusu nakisi ya fedha katika bajeti ya baraza na kumuonya dhidi ya kuwaongeze madiwani mishahara.
- **Viongozi** wa wafanyi kazi walipeleka malalamishi yao kwa Meya akapuuza.

*3 × 2 = 6*

3. Kwa kutoa mifano kumi, eleza vizingiti walivyokumbana navyo wanacheneo wakati wa kupigania mageuzi.

- Vitisho kutoka kwa Mstahiki Meya na vibaraka wake hasa dhidi ya wafanyakazi waligoma, ambao wanatishiwa kufutwa kazi.
- Waandamananji na waliopinga uongozi wa Mstahiki Meya wanapigwa (kutembezwa virungu) mpaka wanatulia nyumi.
- Waandamanaji wanashambuliwa na bunduki (risasi) vitoa machozi na magari yanayotapika maji.
- Mwandamanaji akifa, viongozi wanasema hakuna aliyekufa (uk 65)
- Vibaraka kama vile Diwani I, II na Bili kuendeleza ushauri potovu kwa Meya na kuwafanya wananchi waumie hata zaidi.
- Usaliti wa viongozi wakisiasa waliowachangua (Meya na Madiwani) ambao badala ya kuleta maendeleo, wanatumia nyadhifa zao kuwanyanyasa raia hata zaidi.
- Askari wanatumiwa kukandamiza raia hasa walioandamana.
- Ubinafsi wa Mstahiki Meya na vibaraka wake wakijilimbikizia mali na kushiriki ufisadi ni mzigo kwa wananchi kwa sababu pesa za maendeleo zinaibwa na wanasukumwa katika umaskini zaidi.
- Kazi zinapotokea katika baraza zinapaswa kutangazwa wazi ili walio na tajriba na waliosomea kazi hiyo kuhojiwa, na anayestahili zaidi anapta lakini mhazili aliajiriwa kwa mapendeleo.
- Ujinga ni changamoto kwa ukombozi kwa sababu anayehusika hajui haki yake, hajui kusoma nakuandika mf. Mamake Dadavuo Kaole hajui lishe bora ni nini na hajui utapia mlo ni nini na husababishwa na nini.
- Tenga tawala - kugawa wananchi kitabaka (watawala na watawaliwa)
- Matumizi ya propaganga na unafiki unawafanya wananchi kuamini mambo ya uzushi Mf. Waridi anaamini Meya ameagiza dawa kutoka ng'ambo.
- = Matatizo ya afya yanayotokana na ukosefu wa maji safi, mrundiko wa takataka n.k unatishia maisha ya wanacheneo kwa magonjwa kama kipindupindu.
- Baadhi ya wanacheneo wanakataa kuzinfuka. Mf. Gedi anazidi kumnyenyekea Meya bila kujua kuwa Meya ni haini asiyestahili

hehsima.
*zozote 10 × 2 = 20*

4.i) Walemavu hawapati malezi yanayowastahiki kwani wanadumishwa kwa kufungwa.
ii) Matajiri wanawalazimisha maskini kuchangia masomo ya watoto wao k.m. masomo ya Madhubuti.
iii) Watu k.m Yusufu na Amani kufiwa jela bila kosa.
iv) Mtemi anamdhulumu Zuhurua kwa kumpa talaka kwa kumshuku ana uhusiano wa Amani.
v) Mtemia anaghushi faini na kunyakua mashamba ya watu k.m Chichiri Hundi.
vi) Mtemi kupanga mauti ya Chichiri.
vii) Mashujaa kama matuko weye na Chwechwe Makweche kutotambuliwa.
viii) Majisifu kutohudhuria baadhi ya vipindi.
ix) Wagonjwa k.m uhuru kutotibiwa na wauguzi.
x) Mtemi kutolea raia hotuba kwa kiingereza badala ya kiswhaili.
xi) Wanatomoko kulazimishwa kuhudhuria sherehe za sikukuu ya wazalendo.
xii) Gazeti la Tomoko huchapishwa picha ya Mtemi kwa sababu nduguye ni mhariri.
xiii) Mtemi hachanji mbwa wake ilhali anawatoka raia kuwachanja mbwa wao.
xiv)Mtemi kuwafuta watu kazi apendavyo.
xv) Mtemi kuwalipa wafanyikazi mshahara duni.
*zozote 10 × 2 = 20*

**5.a)** Msemaji ni imani.
Msemewa ni Amani.
Walikuwa kwa Amani.
Ni punde baada ya sherehe ya amu yake.
Amani kuachiliwa huru, Imani anamshajisha.
*4 × 1 = 4 marks*

**b)** i) Msemo / Nahau - usimweke pembeni.
ii) Tashbihi - usimweke pembeni **kama** tanbihi.

***Moja - peke (ya kwanza)***
***Kutaja - alama 1***
***mfano - alama 1***

**c)**i) Wenye utu - k,m Imani kuwatunza walemavu.
ii) Ni katili - k.m. Lowela kutupa matoto akake.
iii) Walezi wema - Imani kuwalea vyema watoto walemavu wa majisifu.
iv) Walezi wabaya - k.m. Lowela kukosa kuwajibika kama mzazi. Amtupa mwanawe.
v) Ni waadilifu k. m Imani anajitunza na kutoshiriki mapenzi na Amani.
vi) Wapenda anasa k.,m Lowela.
vii) Jasiri k.m. Dora anajibizana kujasiri na majisifu kuhusu kulaza damu kwake.
viii) Wenye bidii -k.m Imani afanya kazi kwa bidi ikwa majisifu.
ix) Wenye wivu - Bi Zuhura anawaonea wivu wanawake wengine maskini lakini wanaopewa haki yao ya kimapenzi.
*zozote 7 × 2 = 14*

**6.a)** Msemaji ni kananda.
- Msemewa ni Mwatela.
- Wako nyumbani kwa Mwatela.
- Kananda alikuwa ameambulia ujauzito na alitaka kuolewa na Mwatela.
*4 × 1 = 4*

**b)** Ni mwenye vitisho. Anamtisha Kamanda.
- Ni katili.
- Ni mdanganyifu.
- Ni mlevi.
- Ni tajiri.
- Ni mwenye bidii.
- Ni mwenye majuto
- Ni msinzi.

***za mwanza 4 × 2 = 8***
***(aeleze kila hoja) - kwa kutoa mfano.***

**c)** Anapigwa
- Dhuluma za kimapenzi.
- Ajira wakiwa wadogo.
- Wanadanganywa.
- Wananyanganywa mtoto.
- Wanauzwa kama watumwa.

- Wanapata vitisho kutoka kwa wanaume.
- Wanawake kuwa na wanaume wasinzi.
- Hawana usemi mbele ya wanaume.

*zozote 4 × 2 = 8*

***(aeleze kila hoja kwa kutoa mfano)***

7.i) Esther kuwa na shaka iwapo kamata angempisha kiti kama yule kijana ndani ya basi.

ii) Esther kuwa na Shaka Grace atambadilisha Zamu kama alivyoahidi.

iii) Abiria kuwa na shaka ikiwa matatu zilikuwa zinaingia katika uwanja wa ndege.

iv) Esther kuwa na shaka kama Kamata anamjali jinsi yeye Esther anamjali.

v) Esther ana shaka kama Kamata yuko kazini kwa vile hakuwa amemwona.

vi) Esther ana shaka ya kufika Dubai kwa muda.

vii) Esther ana shaka ya uhusiano wa Kamata na Grace.

viii) Esther ana shaka iwapo Kamata ataweza kumpata na kumtambua mteja aliyeacha pesa.

ix) Esther kuwa na shaka kama angepata uhuru aliotaka wa kutaka kuja kutembea Nairobi.

x) Esther kuwa na shaka kama tapata nafasi ya kujifunza usekritari.

*zozote 10 × 2 = 20*

**8. a) Methali** **Vitendawili.**

i) Hazina fonyula maalum wakati wa uwasilishaji wake.
i) huwa na fonyula maalum katika uwasilishaji

ii) Husema na mtu mmoja tu.
ii) Huhitaji watu wawili katika uwasilishaji wake

iii) Hushirikishwa katika vipera vingi na kama nyimbo.
iii) Havishiri kishwi katika vipera vingine

iv) Sana sana hutolewa na wazee.
iv) Huhusisha watoto na vijana

v) Ni fumbo ambalo si lazima lifumbuliwe papo hapo.
v) Fumbo lazima lifumbuliwe papo hapo

***za mwanzo 3 × 2 = 6***

**b)**

i) Tamasha za muziki shuleni.

ii) Tamasha za drama shuleni.

iii) Michezo ya kuigiza katika runinga na vituo vya redio.

iv) Ngoma za kinyeji huchezwa katika hafla mbalimbali.

v) Sherehe mbalimbali harusi, mazishi katika jamii.

vi) Vipindi vya watoto katika runinga na Vituo vya redio.

vii) Utambaji bado unaendelea katika sehemu za mashambani baadhi ya jamii.

viii) Watafiti bado wantatafiti kuhusu fasihi simulizi. ***zozote 3 × 2 = 6***

**c)** i) Ni utanzu wa fasihi simulizi unaohusisha mazungumzo yanayoambatana na matendo. (alama 2)

ii)- Ishara za uso, mwili na miondoko ambayo inaoana na hali ya kuigiza.
- Avalie maleba yanayochukuana na nafasi anayoigiza.
- Abadilishe toni na kiimbo kulingana na hali tofauti.
- Abadalisha vigizaji wake kulingan na hadhira.
- Atumie lugha kwa ufasaha.
- Awe jasiri mbele ya hadhira yake.
- Ashirikishe hadhira yake.
- Awe na uwezo wa ufaraguzi.
- Lazima aelewe tamaduni wa hadhira yake.

***zozote 3 × 2 = 6.***